CHUO KIKUU CHA AFYA
NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI

# HOMA YA DENGUE

## Homa ya Dengue ni nini?

Homa ya Dengue Homa ya dengue ni ugonjwa unaosababishwa na kirusi ambacho kinaenezwa na mbu wa aina ya Aedes

Homa ya dengue inaweza kusababishwa na yeyote kati ya aina nne za kirusi cha dengue yaani: DEN-1, DEN-2, DEN-3, and DEN-4. Unaweza kupata uambukizi wa wa angalau aina mbili kama sio aina zote nne katika nyakati tofauti za maisha, lakini ni mara moja tu kwa kila aina.

## Historia na Takwimu

Ugonjwa huu umejulikana na wataalamu wa afya kwa takribani miaka 200 sasa, Dengue in ugonjwa uliosambaa duniani kote hasa katika nchi za ukanda wa joto kama vile visiwa vya Karibbean, Amerika ya kusini na kati, Afrika, mashariki ya mbali ya Asia na China, India, Mashariki ya kati, na Australia. Takribani asilimia 40 ya watu wote duniani wanaishi katika nchi zenye ugonjwa huu. Takwimu za Shirika la Afya Duniani zinathibitisha kuwa takribani matukio milioni 5 ya Dengue yanatolewa taarifa kila mwaka. Watu wapatao laki 5 hulazwa hospitali kwa kuathirika na Dengue kali. Homa ya Dengue imeshatokea katika nchi zipatazo 34 barani Afrika. Hapa Afrika Dengue ni ugonjwa unaojulikana kwa kiwango kidogo sana. Licha ya kwamba milipuko ya kwanza imetokea tangu mwanzoni wa karne ya 19. Matukio ya Ugonjwa huu yameongezeka Afrika tangu miaka ya 1980, matukio mengi yakitokea nchi za ukanda wa Mashariki mwa Afrika ikiwa ni pamoja na Msumbiji, Somalia, Kenya, Komoro, Djibouti na Tanzania. Ikumbukwe kuwa jina "Dengue" linatokana na neno "Dinga" la kiswahili linalolomaanisha ugonjwa unaotakana na pepo yaani Kudinga pepo. Mabaharia wa Kispanish walipokuja kwenye pwani ya Afrika Mashariki walirudi kwao na kuuita "Dengue"

Aidha, mlipuko wa ugonjwa huu si mpya hapa nchini kwani uligundulika kwa mara ya kwanza mnamo Juni 2010 mkoani Dar es Salaam ambapo idadi ya watu 40 walithibitika kuwa na ugonjwa. Pia, kati ya mwezi Mei hadi Julai 2013,wagonjwa 172 walithibitishwa kuugua ugonjwa huu.

## Uambukizi

Kirusi cha homa ya Dengue kinaambukizwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kwa kuumwa na mbu wa Jamii ya Aedes, na hasa Aedes aegypti. Mbu huyu anaishi katika mazingira ya makazi ya binadamu. Huuma wakati ya mchana ndani ya nyumba au kwenye maeneo yenye vivuli, hususani majira ya asubuhi na jioni kabla jua halijazama. Mbu huyu anazaliana katika maji yaliyotuama hasa kwenye vyombo vya nyumbani, makinga maji ya paa za nyumba, matairi ya gari, ndoo, vikopo, na kadhalika. Kwa bahati mbaya mbu huyu huweza kuzaliana katika vifaa vidogo vidogo ambavyo watu wengi huvidharau. Hivi ni pamoja na makopo ya kuotesha maua, vikombe, vifuu vya nazi, na